# SERA YA MAENDELEO YA USHIRIKA 2002

YALIYOMO

## SURA YA KWANZA


Ukurasa

DIBAJI……………………………………………………….. vi-viii

1.0 UTANGULIZI…………………………………………….. 1

1.1 Usuli………………………………………………. 1
1.2 Vikwazo katika Maendeleo ya Ushirika….. 2
1.3 Sababu za Kuipitia upya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997………….. 4
1.4 Dira ya Jukumu Kuu la Ushirika…………… 5
1.4.1 Dira ya mfumo wa Ushirika………… 5
1.4.2 Jukumu Kuu la Ushirika……………… 6
1.5 Madhumuni Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2002……………………………………………….. 7


## SURA YA PILI


2.0 DHIMA YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MAENDELEO YA TAIFA……………………………….. 8

2.1 Malengo na Madhumuni ya Taifa………….. 8
2.2 Umuhimu wa Ushirika katika Maendeleo ya Taifa…………………………………………………. 9
2.3 Ushirika na Upunguzaji Umaskini ………….. 9
2.4 Ushirika katika Sekta mbalimbali…………….. 10


## SURA YA TATU


3.0 MAADILI NA MISINGI YA VYAMA VYA USHIRIKA 11

3.1 Maadili na Misingi ya Ushirika……………….. 11
3.2 Wanawake na makundi mengine katika

Ushirika ................................................... 14
3.3 Ushirika na Mazingira ............................... 15

## SURA YA NNE

4.0 MUUNDO WA USHIRIKA ................................... 16

4.1 Muundo wa Jumla wa Ushirika.................. 16
4.2 Uanzishwaji wa muundo mlalo wa ushirika Unaonyumbulika..................................... 17
4.3 Uanzishwaji wa miundo wima ya Vyama vya Ushirika ambayo ni imara na inayotekelezeka Kiuchumi.................................................... 17

4.4 Muungano na Mgawanyiko wa Vyama vya Ushirika........................................................ 19

## SURA YA TANO

5.0 UONGOZI NA UTAWALA WA VYAMA VYA USHIRIKA 20

5.1 Uongozi na Ushirika.................................... 20

## SURA YA SITA

6.0 ELIMU NA MAFUNZO YA USHIRIKA..................... 22

6.1 Umuhimu wa Elimu ya Ushirika.................. 22
6.2 Elimu ya Ushirika kwa Wanachama............ 24
6.3 Elimu na Mafunzo ya Ushirika kwa Halmashauri 25
6.4 Elimu na Mafunzo ya Ushirika kwa Watendaji 26
6.5 Elimu ya Ushirika kwa Umma..................... 26

## SURA YA SABA

7.0 ASASI ZA FEDHA KATIKA USHIRIKA ................. 27

7.1 Umuhimu wa Upatikkanaji wa Fedha kwa Ajili ya vyama vya ushirka…………………….. 27
7.2 Vyama vya Akiba ya Mikopo (SACCOS)…. 28
7.3 Benki za Ushirika……………………………… 29
7.4 Uwezeshaji kifedha kwa Vyama vya Ushirika Katika ngazi ya Taifa………………………… 29
7.5 Huduma za Bima ya Ushirika……………….. 31

## SURA YA NANE

8.0 DHIMA YA WATEKELEZAJI WAKUU WA SERA 31

8.1 Ushiiriki wa Serikali katika Shughuli za Ushirika…………………………………………… 31
8.2 Kazi za Asasi za Umma zinazohusika na Maendeleo ya Ushirika……………………….. 33
8.3 Nafasi ya Wahisani katika Juhudi za Kuendeleza Ushirika………………………….. 35

## SURA YA TISA

9.0 UTEKELEZAJI WA SERA ……………………………. 35

## SURA YA KUMI

10.0 HITIMISHO………………………………………………. 36

# DIBAJI

Kama inavyofahamika kwa wengi, Chama cha Ushirika ni "Muungano wa watu waliojiunga pamoja, kwa hiari, kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao kwa kuanzisha na kumiliki chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zake ambazo wao hushiriki kikamilifu"

Katika Vyama vya Ushiirika wanachama wanakuwa na uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yao ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia juhudi zao za pamoja katika kufikia malengo ambayo yasingefikiwa kwa juhudi za mtu mmoja mmoja. Ni kutokana na sababu hii ambapo Serikali inavitambua Vyama vya Ushirika kama vyombo muhimu katika kufikia malengo ya mipango ya maendeleo ambayo huhitaji sana ushiriki wa watu. Kwa kuelewa umuhimu huo. Serikali imekuwa makini katika kuandaa Sera ya Maendeleo ya Ushirika inayoviwezesha Vyama vya Ushirika kuwasaidia wanachama wake na Taifa kwa ujumla katika kufikia malengo ya maendeleo kwa haraka zaidi na hivyo basi kupunguza umaskini.

Sera ya kwanza ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilipitishwa mwaka 1997 kwa ajili ya kutoa malengo ya jumla na mikakati muhimu kuhakikisha kwamba makundi ya watu maskini katika jamii wanakuwa na chombo cha kuaminika cha kuwawezesha kufikia malengo yao ya kiuchumi na kijamii. Mafanikio makubwa yalipatikana kutokana na Sera hiyo. Kwa mfano, maadili na misingi ya ushirika ya kimataifa ilitambuliwa na kufatwa, Vyama vya Ushirika imara ambavyo msingi wake ni wanachama viliundwa na idadi ya Vyama vya Ushirika kwenye sekta mbalimbali za uchumi iliongezeka kwa kiwango kikubwa.

Ingawa Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997 ilipitishwa baada ya mabadiliko katika Sera za kiuchumi, Sera hiyo haikuainisha vya kutosha masuala yanayohusu uchumi wa soko huru, mazingira, jinsia wajibu wa wadau mbalimbali na utandawazi. Hivyo, masuala haya, pamoja na mengine, yamefanya iwe muhimu kuipitia upya Sera ya 1997.

Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002 ina mwelekeo tofauti sana katika ufafanuzi wa wajibu na majukumu ya Serikali na wadau wengine katika kuendeleza na kusaidia maendeleo ya ushirika katika mazingira ya uchumi wa soko huru na utandawazi.

Mambo makuu tofauti katika sera hii yako katika maeneo yafuatayo:-

(a) Sera inaangalia upya majukumu ya Serikali katika kusaidia Vyama vya Ushirika ambavyo vinamilikiwa na kusimamiwa na wanachama wenyewe kwa mujibu wa maadili na misingi ya ushirika inayotambuliwa kimataifa.

(b) Sera inatambua matatizo ya kimuundo na kihistoria ya Vyama vya Ushirika katika mazingira ya uchumi huru, kwa hiyo inaweka mazingira muafaka ili vyama viweze kufanya shughuli kwa ushindani na ufanisi zaidi.

(c) Sera inatambua vikundi vya kiuchumi kama juhudi muhimu za kuelekea kwenye Vyama vya Ushirika halisi ambavyo msingi wake ni wanachama.

(d) Sera inasisitiza kuwepo kwa uongozi wenye mwelekeo na mawazo ya kibiashasra zaidi badala ya uongozi wa kuendesha Vyama vya Ushirika katika utaratibu wenye mwelekeo wa utumishi wa Serikali.

Kwa ujumla Sera inazingatia kero na matatizo ya kihistoria na inakusudia kuanzisha mfumo wa ushirika endelevu unaokidhi mahitaji ya wanachama kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera inatambua umuhimu wa kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika vinavyojitegemea, vinavyohimili ushindani na ambavyo msingi wake ni wanachama na kama vyombo muhimu vya kuviwezesha kiuchumi vikundi vya watu wenye uchumi duni katika jamii na maskini kwa ujumla.

Kwa hiyo lengo kuu la madhumuni ya Sera ni kuhimiza, kusaidia kuendeleza na kupanua wigo wa Vyama vya Ushirika vyenye kuweza kuendelezwa kiuchumi na ambavyo msingi wake ni wanachama.

Ninaamini kuwa katika mazingira ya uchumi wa soko huru Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002 inatoa mwongozo kuhusu majukumu ya Serikali na wadau katika kusaidia na kuendeleza Vyama vya Ushirika ambavyo msingi wake ni wanachama.

Jumanne Maghembe (Mb)
**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Historia ya Vyama vya Ushirika Tanzania inaanzia tangu mwaka 1925 wakati Chama cha Kilimanjaro Native Planters Association kilipoanzishwa. Hata hivyo, Sheria ya kwanza ya Vyama vya Ushirika haikupitishwa hadi mwaka 1932. Baada ya uhuru Sera ya Serikali ilikuwa ni kuufanya ushirika kuwa msingi wa maendeleo ya kiuchumi. Aidha, Azimio la Arusha la mwaka 1967 lilitetea na kuvitambua Vyama vya Ushirika kama vyombo vya utekelezaji wa Sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Kwa kupitia Sheria mbalimbali, ushirika ulipewa nafasi ya kuwa chombo muhimu cha kubadilisha uzalishaji vijijini kuwa uchumi wa kijamaa. Mabadiliko katika Sera za kijumla za kiuchumi, ambayo yalianza mwishoni mwa miaka ya 1980 yaliyokusudia kuanzisha Sera za soko huru na kulegeza masharti ya biashara yalianzisha juhudi zinazoendelea za kuvifanya Vyama vya Ushirika kuwa vya wanachama wenyewe. Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 1991 ilitungwa kwa makusudi hayo. Katika historia ya zaidi ya miaka 70 ya ushirika nchini hapa kuwahi kuwepo na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya kuzilinda Sheria mbalimbali za ushirika hadi mwaka 1997 Sera ya kwanza ya Maendeleo ya Ushirika ilipotayarishwa. Sera hiyo ilisisitiza msimamo wa Serikali katika Maendeleo ya Ushirika kwa kutambua Misingi Mikuu ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani.

### 1.2 Vikwazo katika Maendeleo ya Ushirika

Licha ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997 na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 1991, matatizo katika ushirika yameendelea kuwepo. Kikwazo kikubwa kimekuwa uwezo mdogo wa Vyama vya Ushirika kushindana kibiashara katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Vyama vya Ushirika vilikuwa dhaifu kimuundo na kimtaji wakati wa kuanzishwa kwa Sera za ulegezaji wa masharti ya biashara ambazo ziliianzishwa wakati ambapo Vyama vya Ushirika havikuwa vimejiandaa kukabiliana na mfumo mpya wa uchumi.

Tangu wakati huo Vyama vya Ushirika havijaweza kurekebisha shughuli zake katika mazingira ya ushindani ikilinganishwa na sekta binafsi iliyokuwa imejiandaa vizuri. Vimeshindwa kujirekebisha kimuundo wakati ambapo shughuli zake za kiuchumi zimeendelea kudorora. Matokeo yake

ni kwamba vyama vimeshindwa kutoa huduma zinazoridhisha kwa wanachama wake ambao wameamua kufanya shughuli na wafanyabiashara binafsi.

Kikwazo cha pili kikubwa ni uongozi dhaifu katika Vyama vya Ushirika. Hatua za kuvirekebisha vyama vilivyopo hazikufanikiwa kutokana na tatizo la miundo iliyorithiwa na mielekeo iliyopitwa na wakati na tatizo la kutotaka kuviachia vyama kukua na kuendelea vyenyewe, hivyo basi, kutokuwepo kwa msisitizo katika maendeleo ya ushirika katika msingi wa demokrasia kamili na vyama kumilikiwa na wanachama. Kukosekana kwa usimamizi wa kitaalamu kumesababisha vyama vingi kufanya shughuli ambazo ni vyanzo tu vya mapato kwa viongozi lakini ambazo haziwanufaishi wanachama. Baadhi ya Vyama vya Msingi hufanya shughuli zake kama wakala wa wafanyabiashara binafsi na hukodisha mali au vifaa vyake kwao. Vile vile, Vyama Vikuu vya Ushirika vimeendelea kufanya shughuli ambazo si za manufaa kifedha kama vile vinu vya kuchambulia pamba, vinu vya kusindika mafuta, vyombo vya uchukuzi na hoteli. Kuongezeka kwa matukio ya ubadhirifu wa mali za Vyama vya Ushirika unaofanywa na mameneja na Halmashauri zisizokuwa aminifu ni kikwazo kingine cha Maendeleo ya Ushirika. Kujihusisha kwa viongozi wa kisiasa katika baadhi ya matukio hayo huondoa uwezekano wa kuwashughulikia wahusika kisheria. Kwa upande mwingine, ukosefu wa elimu na mafunzo kwa wanachama unasababisha kutokuwepo kabisa kwa uwajibikaji wa viongozi kwa wanachama.

Mabadiliko ya mazingira ya Vyama vya Ushirika na kupungua kwa majukumu yake katika usambazaji wa pembejeo, uuzaji na usindikaji wa mazao yameacha pengo ambalo wafanyabiashara binafsi hawawezi kuliziba. Vile vile, kutokuwepo kwa Vyama vya Ushirika kumewafanya wazalishaji wadogo wadogo wasiwe na utaratibu wowote wa kufanya shughuli zao kwa pamoja. Katika mazingira ya kiuchumi ya sasa ambapo hali ya upatikanaji wa soko si ya kuridhisha na taarifa kuhusu masoko ni haba, kutomhusisha mkulima mdogo katika shughuli za pamoja ni kumuacha katika hali mbaya. Matokeo ya hali kama hiyo sio tu kwamba yanamuathiri mkulima mmoja mmoja bali pia uchumi wa nchi kwa ujumla.

## 1.3 Sababu za Kuipitia Upya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997

Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997 ilikuwa matokeo ya mabadiliko katika mazingira ya uchumi wa kijumla yaliyosababisha kuanzishwa kwa mfumo wa soko huru na ulegezaji wa masharti ya biashara. Hata hivyo, Sera hiyo haikuzingatia vya kutosha umuhimu wa kuweka mazingira

muafaka kwa Vyama vya Ushirika kufanya shughuli zake na kumudu ushindani katika mfumo mpya wa kiuchumi. Vile vile, Sera haikuzitambua juhudi za vikundi vya kiuchumi vya wakulima/watu vinavyoanzishwa kutokana na nguvu mpya za mahusiano ya uzalishaji (uchumi wa fedha) kama msingi muhimu wa Maendeleo ya Ushirika katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Aidha, Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 1997 haikutoa miongozo kuhusu menejimenti ya vyama ambavyo vingi bado vinaendeshwa kana kwamba bado vipo chini ya mfumo kongwe wa uchumi unaoongozwa na dola. Masuala kama vile jinsia, mazingira, migongano ya kimaslahi kati ya Serikali na wanasiasa kwa upande mmoja na viongozi wa ushirika kwa upande mwingine, katika mazingira ya uchumi wa soko huru na demokrasia ya vyama vingi hayakuzingatiwa vya kutosha. Vile vile, Sera haikuainisha baadhi ya matatizo makubwa ya ushirka kama vile ukosefu wa uaminifu miongoni mwa viongozi na ubadhirifu wa mali za Vyama vya Ushirika. Baadhi ya masuala hayo yameonyeshwa katika ripoti ya Kamati Maalum ya Rais ya mwaka 2000 ya kumshauri kuhusu Kufufua, Kuimarisha na Kuendeleza Ushirika. Wakati ni muhimu kwa Sera ya Maendeleo ya Ushirika kusisitiza juu ya Vyama vya Ushirika kufanya shughuli zake kama vyombo huru vya biashara, ni muhimu vile vile Sera hiyo izungumzie mambo yaliyopita ambayo yalikuwa vikwazo katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## 1.4 Dira na Jukumu Kuu la Ushirika

### 1.4.1 Dira ya Mfumo wa Ushirika

Dira ya mfumo wa ushirika imetoa mwelekeo wa jumla wa Maendeleo ya Ushirika katika siku za usoni utakaoiongoza jamii ya Watanzania kuanzisha mfumo wa ushirika unaokidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii ya wanachama katika kipindi kinachofikiriwa, na katika mazingira yaliyopo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo mwelekeo wa jumla/dira ya mfumo wa ushirika wa Tanzania kwa siku za usoni ni katika kuunda Vyama vya Ushirika imara na endelevu vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya wanachama ya kiuchumi na kijamii.

1.4.2 Jukumu Kuu la Ushirika Katika mazingira ya uchumi wa soko huru, Vyama vya Ushirika ni miongoni mwa watekelezaji wengi wa shughuli za biashara kwenye soko. Wanaushirika wanahitaji vyama vilivyoundwa katika umoja wa vikundi mbalimbali vya wazalishaji wadogo kwa lengo la kuunganisha nguvu za rasilimali zao katika kuendesha shughuli zao za biashara kwa ufanisi ili waweze kuhimili

ushindani wa wafanyabiashara wengine katika soko. Katika hali hii Vyama vya Ushirika vinakuwa chombo cha kuwawezesha kiuchumi watu maskini katika jamii kama vile wazalishaji wadogo wadogo/wakulima, wanawake na vijana ambao, vinginevyo wasingeweza kushindana kwenye soko kama wafanya biashara binafsi. Kwa hiyo, Serikali inaamini kuwa katika mazingira haya, jukumu kuu la ushirika ni kuanzisha na kuendeleza Vyama vya ushirika ambavyo:-

- Msingi wake ni wanachama.
- Vinafanya shughuli zake kiushindani vikiwa vyombo huru vya kiuchumi,
- Vinawajali wanachama wa sasa na wa baadaye.
- Vinafanya kazi kwa manufaa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wenyewe na jamii wanamoishi.

## 1.5 Madhumuni ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002

Kwa kuzingatia jukumu kuu la Maendeleo ya Ushirika, madhumuni makuu ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuhimiza uanzishaji na uendelezaji wa vyama ambavyo vinadhibitiwa na kumilikiwa na wanachama wenyewe.

(ii) Kuhimiza uanzishaji wa vyama imara kiuchumi ambavyo vina uwezo wa kufanya shughuli zake za biashara kwa kujitegemea.

(iii) Kusaidia shughuli za uanzishaji wa vyombo imara vya fedha vya ushirika.

(iv) Kuhimiza uimarishaji wa mtaji katika Vyama vya Ushirika.

(v) Kutambua na kusaidia juhudi za vikundi vya wazalishaji wadogo kwa lengo la kuviwezesha kuwa Vyama vya Ushirika imara kiuchumi baadaye.

(vi) Kulinda shughuli za biashara za ushirika dhidi ya ushindani wa wafanyabiashara binafsi wasiozingatia kanuni na taratibu.

(vii) Kuhakikisha kuwepo kwa uongozi na menejimenti yenye uwezo wa kusimamia ushirika kibiashara na ambayo inawajibika kwa wanachama.

(viii) Kuweka na kuimarisha muundo wa ushirika unaofaa na wenye ufanisi.

(ix) Kusaidia na kuhimiza utoaji wa elimu ya ushirika, mafunzo na huduma za utafiti zinazolenga kwenye uwezeshaji wa wanachama.

(x) Kupanua wigo wa shughuli za Vyama vya Ushirika kwa kuhimiza na kusaidia uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali.

(xi) Kuhimiza shughuli za maendeleo endelevu ya ushirika kwa kuhakikisha kuwa:-

- Wanachama waliopo wanatambua na kuheshimu maslahi ya wanachama wa siku za usoni na yale ya jamii nzima.
- Vyama vya Ushirika vinafanya shughuli zake kwa kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia na hifadhi ya mazingira.

# SURA YA PILI

## 2.0 DHIMA YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MAENDELEO YA TAIFA

### 2.1 Malengo na Madhumuni ya Taifa

Lengo kuu la muda mrefu la maendeleo ya uchumi wa kijamii katika Tanzania kwa kizazi kijacho kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 ni kupatikana kwa maendeleo endelevu ya binadamu. Ushirika ni mojawapo ya nyenzo kuu za kufanikisha dira hiyo. Kauli ya Sera

Serikali itaendelea kuvisaidia na kuvilinda Vyama vya Ushirika kama vyombo muhimu katika kufanikisha malengo ya madhumuni ya Taifa.

### 2.2 Umuhimu wa Ushirika katika Maendeleo ya Taifa

Katika kipindi chote cha historia ya Tanzania ushirika umekuwa chombo muhimu katika maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii. Vyama vya

Ushirika vimeendelea na vitaendelea kuboresha, kwa kiwango cha juu, ushiriki wa wanaushirika kwenye mchakato wa maendeleo ya kiuchumi.

**Kauli ya Sera**

Serikali itaendelea kuhimiza uanzishwaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika kama mojawapo ya nyenzo muhimu katika maendeleo ya watu kiuchumi na kijamii nchini.

## 2.3 Ushirika na Upunguzaji Umaskini

Waraka wa Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini unasisitiza kuwa Serikali itajitahidi kuhakikisha kuwa vyombo vya wananchi maskini kama vile, Vyama vya Ushirika vinakuwa katika mstari wa mbele katika kuanzisha na kuendeleza taratibu na mipango inayofaa kwa kiwango kikubwa na yenye mwelekeo wa soko. Pia wakulima watahamasishwa kuunda vikundi au Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuboresha matarajio yao ya maendeleo kiuchumi na kijamii.

**Kauli na Sera**

Sera ya Maendeleo ya Ushirika inatambua umuhimu ambao Mkakati wa Upunguzaji wa Umaskini unaweka katika maendeleo ya ushirika Serikali itashirikiana na mashirika na asasi zote zinazohusika na upunguzaji wa umaskini ili kuhakikisha mafanikio ya mkakati huo yanapatikana.

## 2.4 Ushirika katika Sekta mbalimbali

Vyama vya Ushirika Tanzania vinajishughulisha zaidi na uuzaji wa mazao ya kilimo. Hali hii imesababisha kutosisitizwa kwa ushirika katika sekta nyingine kama vile fedha, biashara na viwanda, madini, nishati, usafiri na usafirishaji, mawasiliano, maji, uvuvi, nyumba na misitu. Inaonekana hali hii itaendelea kwa muda mrefu licha ya ukweli kwamba mchango wa kilimo katika Pato la Taifa unaendelea kupungua wakati mchango wa sekta zingine umeonesha mwelekeo wa kuongezeka.

**Kauli na Sera**

Serikali inatambua fursa kubwa ya Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali katika kuboresha hali za wazalishaji wadogo kiuchumi na kijamii na hivyo, kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Serikali itahimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali.

Katika kufikia lengo hilo bila kupunguza jukumu la kuhimiza uendelezaji wa Vyama vya Ushirika vya uuzaji wa mazao ya kilimo, Serikali itasisitiza Sera za Maendeleo kwenye sekta nyingine ziutambue ushirika kama nyenzo muhimu ya kufikia malengo yao ya maendeleo.

# SURA YA TATU

## 3.0 MAADILI NA MISINGI YA VYAMA VYA USHIRIKA

### 3.1 Maadili na Misingi ya Ushirika

Katika kuyashughulikia masuala ya Vyama vya Ushirika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mkakati wa Kupunguza Umaskini vinahimiza na kutambua umuhimu wa maadili na misingi ya ushirika kama inavyoelezewa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani. Hii inaonyesha kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kufuata maadili na misingi hiyo katika kufikia malengo na matarajio ya Taifa.

**Kauli na Sera**

Kuhusu maadili na misingi ya ushirika ya Kimataifa Serikali inatambua na kuzingatia:-

(a) Maadili ya ushirika ambayo yamejikita katika kujitegemea, uwajibikaji, demokrasia, usawa, haki na mshikamano na kwamba yatazingatiwa katika juhudi na kuendeleza ushirika kulingana na mazingira ya uchumi wa kijamii ya Tanzania.

(b) Misingi ya ushirika kama mihimili na miongozo muhimu katika utekelezaji wa maadili ya ushirika Misingi hiyo ni:-

**(i) Uanachama wa hiari na ulio wazi**

Vyama vya Ushirika ni vyama vya hiari na uanachama uko wazi kwa watu wote wenye uwezo wa kutumia huduma zake na walio tayari kukubali wajibu na majukumu ya kuwa wanachama bila kubaguliwa kijinsia, kijamii, kimbari, kisiasa au kidini.

**(ii) Wanachama na Udhitibi wa kidemokrasia**

Vyama vya Ushirika ni vyama vya kidemokrasia vinavyoongozwa na wanachama wenyewe ambao kwa vitendo, hushiriki katika malengo yao na kufanya maamuzi. Wale waliochaguliwa kuwa wawakilishi wanawajibika kwa wanachama. Katika Vyama vya Msingi wanachama wana haki sawa katika kupiga kura (kura moja mtu mmoja) na katika ngazi nyingine Vyama vya Ushirika huendeshwa kwa taratibu za kidemokrasia.

**(iii) Ushiriki wa wanachama katika shughuli za kiuchumi**

Wanachama huchangia kwa uwiano wa usawa katika mtaji wa chama chao ambao wanaudhibiti kidemokrasia. Angalau sehemu ya mtaji huo, kwa kawaida huwa ni mali ya jumla ya chama. Kwa kawaida wanachama hulipwa faida kidogo kama ipo kutoka katika mtaji uliochangiwa kama sharti la uanachama. Wanachama hutenga ziada kwa ajili ya madhumuni yafuatayo: kuendeleza chama chao pengine kwa kuweka akiba, ambayo sehemu yake fulani haigawanywi kuwanufaisha wanachama kwa uwiano wa jinsi walivyoshiriki katika shughuli za chama na kusaidia katika shughuli zingine kama itakavyokuwa imeidhinishwa na wanachama.

**(iv) Uhuru na kujitegemea**

Vyama vya Ushirika ni vyombo huru na vinavyojitegemea chini ya uongozi na usimamizi wa wanachama. Iwapo vitaamua kufanya mikataba na vyombo vingine, ikiwemo Serikali au vikiamua kuongeza mtaji kutoka vyanzo vingine vya nje, vyama vitafanya hivyo kwa kuzingatia maamuzi ya wanachama ya kidemokrasia na uhuru wa vyama.

**(v) Elimu, Mafunzo na Taarifa**

Vyama vya Ushirika hutoa elimu na mafunzo kwa wanachama, Halmashauri, Mameneja na watendaji wengine ili waweze kuchangia inavyopasa katika maendeleo ya vyama vyao. Umma kwa ujumla, huelimishwa hususani, vijana na viongozi wahamasishaji kuhusu ushirika ulivyo na manufaa yake.

**(vi) Ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Ushirika**

Vyama vya Ushirika hutoa huduma kwa wanachama wake ipasavyo na huimarisha ushirika kwa kushirikiana kwa kutumia miundo iliyopo katika ngazi ya Chama cha Msingi, Chama Kikuu, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**(vii) Kuijali Jamii**

Vyama vya Ushirika hujihusisha na maendeleo endelevu ya jamii zake kupitia maamuzi ya wanachama wake.

## 3.2 Wanawake na makundi mengine katika Ushirika

Katika mazingira ya sasa ushiriki wa wanawake katika Vyama vya Ushirika ambavyo huongozwa zaidi na wanaume ni kidogo sana. Katika baadhi ya vyama vya mazao wanawake sio wanachama kwa sababu hawamiliki ardhi. Sera na Sheria ya Ardhi vimeangaliwa upya ili kuondoa kasoro hizi za kutokuwepo kwa usawa. Aidha, shughuli za biashara za makundi mengine ya watu (kwa mfano vilema, vijana na wengine) zinaongezeka mjini na vijijini.

### Kauli ya Sera

Ili kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki kikamilifu katika shughuli za ushirika. Serikali itawahamasisha wanawake kuwa wanachama wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa msingi wa hiari na uwazi.

Wanawake watahimizwa kuchukua nafasi za uongozi na ajira katika Vyama vya Ushirika. Serikali itahamasisha Vyama vya Ushirika kuwapatia wanawake upendeleo maalumu katika kupata elimu na mafunzo ya ushirika ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za uongozi na katika kutimiza wajibu wao kwa vyama vyao.

Ili kuongeza ushirika wa makundi yalyowekwa pembezoni katika ushirika shughuli za vikundi hivi zitaainishwa katika mfumo wa ushirika. Vile vile Serikali itavisaidia vikundi hivi ili vipate usajili kamili na kuwa Vyama vya Ushiriika.

### 3.3 Ushirika na Mazingira

Maendeleo endelevu ya ushirika yatategemea jinsi wanachama wanavyozingatia matumizi ya usawa na endelevu ya rasilimali kwa ajili ya mahitaji yao ya lazima ya sasa na ya vizazi vijavyo bila kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama ili Vyama vya Ushirika viweze kuisaidia jamii ni lazima vihakikishe kuwa wanachama wake wanajitahidi kuboresha hali za maisha yao na kufikia viwango ambavyo vinahitajika kijamii na ambavyo ni endelevu kiuchumi na kimazingira.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahimiza Vyama vya Ushirika kuzingatia masuala ya mazingira katika programu zake za maendeleo.

## SURA YA NNE

## 4.0 MUUNDO WA USHIRIKA

### 4.1 Muundo wa Jumla wa Ushirika

Vyama vya Ushirika vimeundwa kiulalo na wima. Tangu ilipotungwa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 1991, Vyama vimekuwa katika mfumo wa ngazi nne zilizo wima ambazo ni Vyama vya Msingi Vyama Vikuu, Vyama Vilele na Shirikisho. Matatizo ya utekelezaji wa mfumo huo yameonesha wazi kuwa hayakutokana na wanachama. Mfumo huo umesababisha, kuongezeka urasimu, utendaji usioridhisha na wanachama kutowajibika. Pia mfumo huu umekuwa wa gharama kubwa kiuendeshaji na hivyo kuwa mzigo usiokuwa wa lazima kwa wanachama hususan, ngazi ya tatu haikutimiza wajibu wake ipasavyo. Kamati Maalum ya Rais ya kufufua. Kuimarisha na Kuendeleza ushirika pia ilibaini mapungufu hayo.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahimiza uanzishwaji wa mfumo wa ushirika unaozingatia gharama nafuu na unaotokana na mahitaji ya wanachama.

### 4.2 Uanzishwaji wa muundo mlalo wa ushirika unaonyumbulika

Muundo wa ushirika wa ulalo ulioko hivi sasa umekuwa na matatizo ya kiutekelezaji. Kwa upande mmoja. Vyama vya Ushirka katika maeneo

makubwa vimekuwa na matatizo ya kuandaa Mikutano Mikuu ambayo imekuwa ya gharama kubwa kiasi cha kutishia uwezo wa kiuchumi wa vyama hivyo. Kwa upande mwingine uanzishwaji wa vyama vinavyochukua maeneo madogo kijiografia umesababisha kuwepo kwa utitiri wa vyama ambavyo haviendesheki kiuchumi.

**Kauli ya Sera**

Serikali itabuni njia za kuhakikisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirka unakuwa na gharama ndogo ili kuwezesha Vyama vya Ushirka kufanya shughuli zake kwa ufanisi katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Serikali itaendelea kusisitiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vyenye uhai wa kiuchumi bila kujali ukubwa wa maeneo yao kijiografia.

## 4.3 Uanzishwaji wa miundo wima ya Vyama vya Ushirika ambayo ni Imara na inatekelezeka Kiuchumi

Vyama vingi vya Msingi vilivyopo haviendesheki kiuchumi kwa sababu ya uchache wa wanachama ambao huchangia mtaji mdogo. Katika vyama hivi wanachama huchangia tu kiwango cha chini cha hisa kinachohitajika. Pia, thamani ya hisa na rasilimali ni za chini mno na haziongezeki au kupungua thamani kulingana na hali ya bei za soko. Mwaka hadi mwaka kumekuwa na ongezeko la idadi ya Vyama Vikuu. Baadhi ya Vyama hivi huanzishwa kwa msingi wa mipaka ya utawala ya Wilaya na Mikoa na sio kwa msingi wa utekelezaji/Uendeshaji wa kiuchumi. Baadhi yake vimekuwa na miundo mikubwa ambayo husababisha kupungua kwa ufanisi katika utendaji. Vingine vimejihusisha na shughuli nyingine za kibiashara ambazo kimsingi si majukumu yake makuu. Hali hiyo imesababisha Vyama Vikuu kuwa mbali na Vyama vya Msingi na biashara ya vyama hivyo imepungua kwa kiasi kikubwa.

**Kauli ya Sera**

Katika juhudi za kuimarisha muundo wima wa Vyama vya Ushirika msisitizo utawekwa kwenye Vyama vya Msingi ili kufikia lengo hilo Serikali:-

(i) Itatambua na kuvisaidia vikundi ambavyo havijafikia hadhi ya kuwa Vyama vya Ushirika kamili kama moja ya hatua muhimu ya uanzishwaji wa Vyama vya Msingi imara.

(ii) Itahimiza uanzishwaji wa Vyama vya Msingi katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

(iii) Itahimiza Vyama vya Msingi kukuza mitaji ya ndani.

(iv) Itahimiza uanzishwaji wa asasi za kifedha katika ngazi za Vyama vya Ushirika vya Msingi.

(v) Itasaidia Vyama vya ushirika vya Msingi katika kupata mikopo kutoka kwenye asasi za fedha za kitaifa na kimataifa.

(vi) Kwa kuzingatia mazingira maalumu itatoa dhamana kwa Vyama vya Ushirika ili kuviwezesha kupata mikopo kutoka kwenye asasi za fedha.

Ni mategemeo ya Serikali kuwa kukiwa na Vyama vya Msingi imara ngazi za juu katika muundo wima wa ushirika zitaanzishwa pale tu zitakapokuwa zinahitajika. Vyama vya Ushirika vitahimizwa kuanzisha biashara za pamoja ili kudumisha na kuendeleza vyama hivyo kiuchumi na kuongeza ufanisi wa shughuli zake. Aidha, Serikali itahimiza utekelezaji shughuli za kibiashara katika ngazi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuvihamasisha Vyama vya ngazi za juu kuwa na majuku ya kuratibu, kushauri na kutoa taarifa kwa Vyama vya Msingi kuhusu hali ya soko. Ngazi ya juu kabisa katika muundo wima wa Vyama vya Ushirika itakuwa ndiyo msemaji mkuu wa ushirika, kitaifa na kimataifa.

## 4.4 Muungano na Mgawanyo wa Vyama vya Ushirika

Hapo awali muungano na mgawanyo wa Vyama vya Ushirika ulikuwa ukifanyika kwa misingi ya kijiografia na kiisiasa badala ya kufanyika kwa msingi ya kiuchumi. Matokeo yake kumekuwa na ongezeko la vyama visivyoendesheka kiuchumi. Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika 1991 yaliyofanyika mwaka 1997 katika kuanzisha muungano au mgawanyo wa lazima hayakusaidia kuondoa tatizo hilo.

### Kauli ya Sera

Ili kutilia mkazo msingi wa uanachama wa hiari na wazi muungano au mgawanyo wa vyama utakuwa wa hiari. Hata hivyo, Serikali inaweza kushauri vyama viungane au vigawanywe ili kuongeza uwezo wake wa kiuchumi na ufanisi pale itakapoonekana inafaa.

## SURA YA TANO

# 5.0 UONGOZI NA UTAWALA WA VYAMA VYA USHIRIKA

## 5.1 Uongozi wa Ushirika

Mfumo wa menejimenti ya ushirika uliopo umeshindwa kuvibadili Vyama vya Ushirika kuwa vyombo imara vinavyoweza kuhimili ushindani wa kibiashara. Aidha kuna mapungufu katika Sera na Sheria zilizopo Matokeo yake ni kuwa viongozi wabovu wameendelea na tabia ya kushikilia nafasi za uongozi bila ukomo wakiendeleza ubovu wa menejimenti katika mfumo wa ushiirka. Hali inakuwa mbaya zaidi kutokana na ukweli kwamba mfumo wa ushirika uliopo haujawa na kanuni za maadili ya uongozi wa ushirika. Vile vile kumekuwepo na mgongano wa kimaslahi. Kwa mfano kumekuwa na baadhi ya viongozi wa Serikali na wa siasa walioko kwenye uongozi wa ushirika kushawishi maamuzi ya Vyama vya Ushirika moja kwa moja au kwa kutumia madaraka yao kinyume na maslahi ya ushirika.

### Kauli ya Sera

Ili kushughulikia matatizo ya uongozi katika ushirika, Serikali itahakikisha kuwa uongozi wa ushirika unakuwa katika misingi ya ujuzi, uaminifu, uwazi, uwajibikaji kwa wanachama demokrasia na kutokuwepo kwa ngongano wa kimaslahi. Kwa mfano Serikali itaweze kuanzisha hatua ambazo zinakusudia:-

(i) Kuanzishwa na kuimarishwa kwa Halmashauri ya Usimamizi ndani ya muundo wa uongozi wa ushirika.

(ii) Kuweka kikomo cha muda wa uongozi katika Vyama vya Ushirika.

(iii) Kuanzishwa kwa kanuni za maadili ya uongozi katika Vyama vya Ushirika ztakazohusu halmashauri na menejimenti.

(iv) Kutenganisha uongozi wa Serikali na kisiasa na ule wa ushirika.

Ufanisi na utekelezaji katika chombo chochote cha kibiashara kunategemea pamoja na sifa nyingine, dira ya Mtendaji Mkuu, ubora wa watendaji na uongozi wa pamoja. Viongozi wa ushirika wanatarajiwa kuajiri watendaji wenye vipaji vya ujasiriamali na wenye uwezo wa kutafsiri dira na mipango ya vyama vyao kwa manufaa ya kiuchumi na

kijamii ya wanachama. Kwa hivi sasa ushirika unahitaji watu wenye viwango vya juu katika uongozi wa Vyama vya Ushirika. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine katika maendeleo ya ushirika, itaendelea kutoa kipaumbele katika maendeleo ya watumishi katika Vyama vya Ushirika.

Ili kuwavutia kuendelea kuwa na watendaji wenye ujuzi, Serikali itahimiza Vyama vya Ushirika kuanzisha na kuendeleza masharti na kanuni za ajira ambazo ni za kuvutia zenye ushindani na zinazozingatia masuala ya maendeleo ya watendaji na taaluma zao.

## SURA YA SITA

## 6.0 ELIMU NA MAFUNZO YA USHIRIKA

### 6.1 Umuhimu wa Elimu ya Ushirika

Elimu na mafunzo ya ushirika ni moja ya misingi ya ushirika. Madhumuni yake ni kuboresha uelewa wa wanachama, viongozi na watendaji katika kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha kuwa umma unauelewa ushirika. Kuanzia miaka ya 1990 msaada wa Serikali katika elimu ya ushirika umekuwa ukipungua kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa upande mwingine, Vyama vya Ushirika vimeshindwa kuziba pengo hilo lililoachwa na Serikali. Matokeo yake ni kwamba elimu ya ushirika imekuwa ikipungua miongoni mwa viongozi wa ushirika, wanachama, watendaji na umma kwa ujumla. Serikali iliporuhusu uchumi wa soko huru, hali iliyolazimisha Vyama vya Ushirika kushindana kibiashara na makampuni binafsi, haikuweka utaratibu wa mafunzo na/au kuviandaa Vyama vya Ushirika kuweza kufanya biashara katika mazingira ya ushindani. Matokeo yake ni kwamba Vyama vya Ushirika viliathirika vibaya kimuundo na kifedha katika kutekeleza shughuli zake. Kutokana na udhaifu huo kiwango cha biashara katika Vyama vya Ushirika kilishuka kwa zaidi ya asilimia 50 katika kipindi kilichofuatia ulegezaji wa masharit ya biashara.

#### Kauli ya Sera

Katika kuzingatia lengo la kuboresha uelewa wa wanachama, viongozi na watendaji katika kutekeleza majukumu yao na kuhakikisha kuwa umma kwa ujumla unaelimishwa kuhusu ushirika ulivyo. Serikali itasisitiza uboreshaji wa elimu ya ushirika kwa lengo la:-

(i) Kuwa na viongozi walioelimika wenye kuwajibika na wenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti kikamilifu shughuli za Vyama vya Ushirka kwa manufaa ya wanachama na hivyo basi kutetea misingi na maadili ya ushirikiano kwa ustawi endelevu wa ushirika na Taifa kibiashara.

(ii) Kutoa elimu muafaka kuhusu usimamizi biashara na stadi za ujasiriamali inayohitajika kwa watendaji na halmashauri kwa ajili ya ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa na Vyama vya Ushirika katika mazingira ya ushindani.

(iii) Kuhakikisha kuwa umma kwa ujumla unaendelea kuelimishwa kuhusu ushirika ulivyo na manufaa yake kwa wanachama.

## 6.2 Elimu ya Ushirika kwa Wanachama

Vyama vingi vya Msingi vinaundwa na watu ambao sio tu kwamba hawana rasilimali za kutosha lakini vile vile hawana maarifa muhimu ya kuwawezesha kuendelea kuwepo na kuhimili harakati za ushindani na utandawazi. Hali hii inahitaji uboreshaji na ukuzaji wa elimu kwa wanachama ambayo itawasaidia katika kufanya maamuzi sahihi na hivyo kuelekeza rasilimali zao adimu kwenye shughuli za kibiashara zenye faida na kuwachagua Halmashauri wenye uwezo. Hatua hii itasaidia Vyama vya Ushirika kuwa na uwezo mkubwa wa ushindani katika biashara.

### Kauli ya Sera

Serikali itahakikisha kuwa elimu ya ushirika katika ngazi ya wanachama inalenga katika kuwa na wanachama walioelimika na waaminifu. Kwa hiyo, msisitizo wa elimu utakuwa katika shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa kiushirika, kazi na wajibu wa wanachama na manufaa ya kuwa mwanachama wa ushirika. Aidha, wakati wa kuchagua wajumbe wa Halmashauri mkazo wa pekee utakuwa katika kuhimiza wanachama kuchagua watu waaminifu, wawajibikaji na walioelimika.

## 6.3 Elimu na Mafunzo ya Ushirika kwa Halmashauri

Wanachama wa Chama cha Ushirika huwachagua wanachama wachache kati yao kushiriki katika kufanya maamuzi na usimamizi wa shughuli za kila siku za chama. Hivyo ni muhimu wajumbe wa Halmashauri

waelimishwe kuhusu shughuli za Chama cha Ushirika ili waweze kuweka sera na mkakati kwa ajili ya maendeleo ya chama.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahakikisha kuwa elimu na mafunzo kwa Halmashauri vinalenga katika kuboresha uwezo wao wa kuendesha biashara katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Serikali inaweza kutoa elimu na mafunzo katika maeneo kama vile:-

(i) Muundo wa ushirika.

(ii) Mazingira ya kibiashra ambamo chama cha ushirika kimo au jukumu lake kuu

(iii) Utoaji wa huduma bora kwa wanachama.

(iv) Mazingira ya ushirika, uongozi na stadi za ujasiriamali na

(v) Utaalamu katika kuajiri watendaji wa kada zote

Katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo msisitizo wa pekee utawekwa katika kufundisha nidhamu ya uongozi na kuhakikisha matokeo kazi kutoka kwa watendaji yanaonekana.

## 6.4 Elimu na Mafunzo ya Ushirika kwa Watendaji

Watendaji waliopo wa Vyama vya Ushirka hawana sifa na stadi za ujasiriamali zinazotakiwa katika kutafsiri sera na mikakati ya ushirka ili kupata matokeo yanayotarajiwa kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Mara nyingi kuajiriwa kwao hufanyika bila kuzingatia sifa na hata baada ya kuajiriwa hakuna mafunzo kazini ya kutosha.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahimiza na inapokuwa lazima itasaidia kuajiri wataalamu wenye sifa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika na kuendesha mafunzo kazini.

## 6.5 Elimu ya Ushirika kwa Umma

Utoaji wa elimu ya ushirika hautakamilika bila kuhusisha umma ambao watu wake mijini na vijijini wana viwango mbalimbali vya elimu. Utoaji wa

elimu kwa umma na asasi za mafunzo ni jambo muhimu katika maendeleo ya Vyama vya Ushirika imara vya siku za usomi na vyenye wanachama wenye moyo.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahimiza utoaji wa elimu ya ushirika kwa umma katika ngazi zote kwa ajili ya kuwa na Vyama vya Ushirika imara katika siku za usoni. Maudhui ya elimu hii yanaweza kuwa pamoja na:-

(i) Chama cha Ushirika kama asasi ya kibiashara.

(ii) Shughuli za Chama cha Ushirika.

(iii) Manufaa kwa wanachama na

(iv) Maadili na sifa maalumu za ushriika kama vile usawa haki na ushirikiano kwa manufaa ya wote.

Aidha, Serikali itahimiza kuingizwa kwa elimu ya ushirika kwenye mitaala na katika mfumo wa Elimu ya Taifa.

Katika juhudi ya kuwa na watumishi waliofunzwa vizuri ambao wataweza kusimamia Vyama vya Ushirika katika mazingira ya uchumi wa soko huru. Serikali itahimiza uanzishwaji wa asasi za mafunzo ya ushirika hadi ngazi ya Chuo Kikuu.

# SURA YA SABA

## 7.0 ASASI ZA FEDHA KATIKA USHIRIKA

### 7.1 Umuhimu wa Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Vyama vya Ushiriika

Asasi za fedha ni vyombo muhimu sana katika maendeleo ya ushirika Asasi za fedha, ambazo zinaanzishwa kama Vyama vya Ushirika ni mbadala wa mifumo mingine ya benki za biashara na zinaweza kutumika katika kuhimiza uangalifu katika matumizi ya fedha na kujenga tabia ya kuweka akiba kwa wanaushirika. Asasi za fedha katika ushirika, vile vile, ni chanzo cha mikopo kwa wanachama na vyama vingine vya ushirika kwa kuwa na masharti nafuu ya ulipaji wa mikopo ukilinganisha na benki nyingine za biashara. Asasi za fedha katika ushirika zinasaidia pia kuhifadhi fedha za wanaushirika ndani ya mifumo wa ushirika kwa

manufaa ya wanaushirika wenyewe. Kwa hiyo katika hali ya sasa ambapo Vyama vya Ushirika huonekana kuwa havikopesheki kwa mujibu wa vigezo vya benki nyingine za biashara uanzishwaji na uendelezwaji wa asasi za fedha za ushirika ni jambo lisiloepukika kwa maendeleo ya ushirika Tanzania.

**Kauli ya Sera**

Serikali itahimiza uanzishwaji wa asasi za fedha katika ushirika kwa ajili ya kufufua tabia ya kuwa waangalifu katika matumizi ya fedha na kujenga tabia/ari miongoni mwa wanachama ya kuweka akiba hivyo kuwezesha Vyama vya Ushirika kunufaika kutokana na mtaji utakaozalishwa.

## 7.2 Vyama vya shirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS)

Katika kipindi kilichopita uanzishwaji wa SACCOS vijijini ulikuwa unakwenda polepole. SACCOS nyingi zilianzishwa mijini na sehemu za kazi. Matokeo yake ni kuwa wanachama wa Vyama vya Msingi vya mazao hawakuweza kuweka akiba ya fedha ambazo zingewawezesha kununua hisa na hivyo kuongeza mtaji wa vyama vyao. Kwa upande mwingine, Vyama vya Msingi vyenyewe vilishindwa kupata mikopo kwa ajili ya kukusanya mazao na kununua pembejeo kwa ajili ya wanachama wao.

**Kauli ya Sera**

Ni kutatua tatizo la ukata kwa wanachama na Vyama vya Ushirika vya Msingi. Serikali itahimiza uanzishwaji wa SACCOS katika maeneo ya shughuli za Vyama vya Msingi. Vile vile, Serikali itaendelea kutoa misaada ya kitaalamu ili kuimarisha na kuendeleza SACCOS zilizoko mijini na vijijini.

## 7.3 Benki ya Ushirika

Kasi ya uanzishwaji wa benki za ushirika imekuwa ndogo. Pamoja na umuhimu wa benki hizi katika maendeleo ya ushirika kiuchumi ni benki chache tu ambazo zimekwishaanzishwa hadi sasa. Pia ndani ya mfumo wa ushirika kuna upungufu wa wataalamu wa kutosha kwa ajili ya uanzishwaji wa benki za namna hii.

**Kauli ya Sera**

Serikali pamoja na wanaushirika bado wanaona kuwa uanzishwaji wa benki hizi ni njia muhimu katika kutatua matatizo ya kifedha katika Vyama vya Ushirika. Katika juhudi za kuwa na mfumo endelevu wa upatikanaji

wa fedha kwa ajili ya Vyama vya Ushirika. Serikali itaendelea kuhimiza na kusaidia uanzishwaji wa benki za ushirika.

## 7.4 Uwezeshaji kifedha kwa Vyama vya Ushirika katika ngazi ya Taifa

Baada ya ubinafsishaji wa asasi za fedha, juhudi za moja kwa moja za Serikali za kutoa fedha kwa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wanachama zilisitishwa. Kwa upande mwingine benki za biashara zinasita kutoa mkopo kwa Vyama vya Ushirika hasa kwa sababu wafanyabiashara wa kati ambao hupandisha gharama za ukusanyaji na uuzaji wa mazao na hivyo kupunguza faida kwa wakulima wameitumia hali hii kujinufaisha kwa kuwabebesha gharama kubwa wakulima wadogo.

### Kauli ya Sera

Kwa kutambua umuhimu wa Vyama vya Ushirika katika ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wakulima. Serikali itachukua hatua za muda mfupi na mrefu ili kupata ufumbuzi wa tatizo la ukosefu wa mtaji kwa Vyama vya Ushirika.

Katika kipindi cha muda mfupi, Serikali itasaidia mipango ya kuvipatia Vyama vya Ushirika fedha ili kuvipa uwezo wa ushindani katika ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wanachama kwa kutumia mbinu bora za usimamizi na uongozi wa biashara. Serikali itashirikiana na benki za biashara katika suala hili.

Serikali inaelewa kuwa hatua za muda mfupi hazitoshelezi katika kupata mitaji endelevu inayokidhi mahitaji ya fedha kwa ajili ya ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya wanachama. Aidha benki za ushirika zinaweza zisiwe na fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya vyama vyote vya ushirka katika kipindi fulani kutokana na matatizo ya kijiografia na upatikanaji wa fedha za kutosha. Ili kuhakikisha kuwepo na upatikanaji endelevu wa fedha za mikopo kwa Vyama vya Ushirika. Serikali itahimiza na kusaidia Vyama vya Ushirika kuanzisha utaratibu endelevu wa kupata fedha kama hatua ya muda mrefu. Juhudi hivi zinaweza kuhusu pia uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ya Taifa.

### 7.5 Huduma za Bima ya Ushirika

Vyama vya Ushirika kwa kutumia Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania, vimekuwa vinafanya shughuli za uwakala wa bima kwa niaba ya Shirika la Bima la Taifa . Katika mazingira ya soko huru katika biashara ya bima, Vyama vya Ushirika vitanufaika zaidi kama vikianzisha asasi za bima ya ushirika.

**Kauli ya Sera**

Ili Vyama vya Ushirika viweze kunufaika kutokana na kuanzisha mfumo wa soko huru katika biashara ya bima. Serikali itahimiza na kusaidia uanzishwaji wa Asasi za Ushirika zitoazo Huduma ya Bima.

## SURA YA NANE

## 8.0 DHIMA YA WATEKELEZAJI WAKUU WA SERA

### 8.1 Ushiriki wa Serikali katika Shughuli za Ushirika

Serikali ilianza kujihusisha katika masuala ya ushirika mara baada ya kupitishwa kwa Sheria ya kwanza ya Vyama vya Ushirika mwaka 1932. Awali kujihusisha huko kulifanyika kwa kupitia Mrajis wa Vyama vya Ushirika ambaye madaraka yake yalihusu uhamasishaji uandikishaji, ukaguzi na ufutaji wa Vyama vya Ushirika. Kuanzia wakati huo Serikali imekuwa ikisaidia katika utekelezaji wa ushirka kwa njia mbalimbali kwa mfano kwa kusaidia Vyama vya Ushirika kupatia mitaji uwezeshaji katika mafunzo na uanzishwaji wa asasi za mafunzo ya ushirika na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

**Kauli ya Sera**

Mwelekeo wa maendeleo ya uchumi unaonyesha kwamba ukuaji na maendeleo ya ushirika kwa siku za usoni yatapatikana kutokana na ari binafsi ya maendeleo na ushiriki wa wanachama. Aidha, kutokana na Sera za uchumi wa soko huru na ubinafsishaji wa biashara, hali ambayo imefanya Serikali ijitoe kwenye shughuli za biashara hivyo kupungua kwa misaada ya kitaalamu na kifedha kwa Vyama vya Ushirika kutoka Serikalini. Serikali itahimiza uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika kulingana na mfumo wa uchumi uliopo ili kuviwezesha kutoa huduma bora na kwa ufanisi kwa wanachama wake kutokana na juhudi na rasilimali zao wenyewe.

Serikali itahakikisha kuwa katika siku za usoni juhudi zake katika maendeleo ya ushirika zitalenga katika kuweka mazingira muafaka katika uanzishwaji na uendelezwaji wa Vyama vya Ushirika ambavyo vinajitegemea, vinavyoundwa na kuongozwa kwa misingi ya kidemokrasia, vyenye kuendesheka kiuchumi na vinavyomilikiwa na wanachama kulingana na maadili na misingi ya ushirika inayokubalika Kimataifa.

## 8.2 Kazi za Asasi za Umma zinazohusika na Maendeleo ya Ushirika

Kwa mujibu wa sera za uchumi za kijumla na za maendeleo ya ushirika, kazi za asasi za umma zinazohusika na maendeleo ya ushirika ni kama ifuatavyo:-

### Wizara yenye dhamana ya Ushirika

Kimsingi kazi kuu ya Wizara husika ni kusimamia na kuwezesha kuwepo kwa mazingira muafaka katika maendeleo ya Vyama vya Ushirika vinavyojiendesha na kujitegemea vyenyewe. Hivyo, Wizara itahusika na:-

(i) Kuandikisha, kufuta na kusimamia ufilisi wa Vyama vya Ushirika;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

(iii) Kutayarisha Sera na mikakati ya maendeleo ya ushirika;

(iv) Kuajiri wakaguzi wa Vyama vya Ushirika wenye sifa zinazostahili;

(v) Kutoa huduma za ushauri na kuweka mazingira muafaka yatakayowezesha ukuaji na uendelezaji wa ushirika.

(vi) Kuhimiza na kusaidia utafiti katika maendeleo ya ushirika;

(vii) Kufanya uchunguzi na ukaguzi kuhusu uendeshaji wa shughuli za ushirika;

(viii) Kuhakikisha kuwa kesi zinazohusisha Vyama vya Ushirika zinashughulikiwa kwa haki na kwa haraka.

**Wizara Nyingine/Idara za Serikali**

Serikali inatambua ukweli kuwa Vyama vya Ushirika huendesha shughuli zake katika maeneo ambayo yanaweza kuwa chini ya usimamizi na ukuzaji wa Wizara nyingine na Idara mbalimbali za Serikali. Baadhi ya Wizara na Idara hizo za Serikali ni pamoja na Wizara zinazohusika na Kilimo, Fedha, Serikali za Mitaa, Viwanda na Biashara Maendeleo ya Jamii, Nishati na Madini na Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Serikali itahkikisha kuwa Wizara na idara hizo zinashirikiana na Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Ushirika kwa lengo la kufanikisha Maendeleo ya Ushirika nchini.

**Chuo cha Ushirika Moshi**

Chuo cha Ushirika Moshi na matawi yake ni asasi ya Serikali inayohusika na utoaji wa elimu na mafunzo ya ushirika. Hivyo majukumu yake ni:-

(i) Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya ushirika;

(ii) Kuandaa na kuendesha programu za elimu na mafunzo ya ushirika na

(iii) Kufanya utafiti na kutoa ushauri kuhusu Maendeleo ya Ushirika.

**Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)**

Katika mazingira ya uchumi wa soko huru Vyama vya Ushirika vinahitaji usimamizi imara wa shughuli zake za biashara. Pamoja na mambo mengine hili linaweza kufanyika kwa kuhakikisha kuwa hesabu za Vyama zinatunzwa vizuri na kuhakikisha kuwa hatua zinazostahili zinachukuliwa pale ambapo dosari zinaonekana. Hivyo jukumu kuu la COASCO ni kufanya ukaguzi na kusimamia hesabu za Vyama vya Ushirika. Hata hivyo Makampuni au Mashirika binafsi ya ukaguzi yanaweza kuruhusiwa kuwa wakaguzi wa Vyama vya Ushirika.

## 8.3 Nafasi ya Wahisani katika juhudi za Kuendeleza Ushirika

Katika kuweka mazingira muafaka ya maendeleo ya ushirika. Serikali itawezesha Vyama vya Ushirika kupata misaada kutoka kwa wahisani. Hata hivyo, Vyama vya Ushirika vitahimizwa kufanya mipango yake ya kuwasiliana na jumuiya ya wahisani pamoja na vyama vingine vya ushirika

kitaifa na kimataifa katika masuala ya fedha za kitaalamu. Pale itakapokuwa lazima Serikali itaratibu na kusimamia juhudi hizo za kusaidia ushirika.

## SURA YA TISA

## 9.0 UTEKELEZAJI WA SERA

Mafaniko ya malengo ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2002 yanategemea mambo muhimu mawili:-

(i) Kuwapo kwa Mikakati ya utekelezaji wake;

(ii) Sheria ya Vyama vya Ushirika

Inatarajiwa kwamba utekelezaji wa Sera hii utaanza mara tu baada ya kuchapishwa kwake na kwamba wahusika wote wataanza kuchukua hatua kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wake. Mkakati wa utekelezaji na Sheria vitaandaliwa kwa ajili ya kutoa maelekezo zaidi katika utekelezaji.

## SURA YA KUMI

## 10.0 HITIMISHO

Sera hii imeainisha umuhimu wa kuweka mazingira muafaka ambamo Vyama vya Ushirika vitaweza kufanya shughuli zake kwa mafanikio katika mazingra ya Sera za uchumi wa kijumla za mfumo wa soko huru na ulegezaji wa masharrti ya biashara. Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Maalum ya Rais mwaka 2000 kuhusu Ufufuaji, Uimarishaji na Uendelezaji wa Ushirika yamezingatiwa katika Sera hii. Vyama vya Ushirika vinatarajiwa kutumia nafasi iliyopo ya mazingira muafaka ili kuwahudumia wanachama wake ipasavyo. Ni matarajio ya Serikali kwamba kuwepo kwa Vyama vya Ushirika imara, endelevu na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama kiuchumi na kijamii, ambalo ndilo lengo la Sera hii kutakuwa na tija kubwa katika maendeleo ya uchumi wa Taifa

Kutokana na hali hiyo Vyama vya Ushirika vinatarajiwa kufanya shughuli zake kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya wanachama wake kijamii na kiuchumi kulingana na maadili na misingi ya ushirika ya kimataifa, hususani msingi wa kujali jamii katika maeneo ambamo wanafanya shughuli zao na nchi kwa ujumla.